

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**



**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE**

**23 MEI, 2022**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 23 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 238. MHESHIMIWA SYLVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mji wa Kibaha utakuwa Manispaa.

#### 239. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Fedha za Mfuko wa Jimbo zinaweza kutumika kununulia Samani za Ofisi ya Jimbo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**240. MHESHIMIWA MOHAMED SULEIMAN OMAR (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa kupitia upya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na kuuongezea Fedha kwa upande wa Zanzibar.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**241. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini mkongo wa mawasiliano wa Taifa utapelekwa katika Wilaya 14 ikiwemo za Mjini Magharibi na Kusini Unguja.

**WIZARA YA MAJI:**

**242. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN  
ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa maji msereko wa Kiburubutu Ifakara utakamilika.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**243. MHESHIMIWA ASSA NELSON MAKANIKA  
(KIGOMA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara ya Mwandiga hadi Manyovu Mkoani Kigoma.

**244. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR  
(NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-


Je, ni lini ahadi ya Waziri Mkuu ya ujenzi wa Barabara ya Kharumwa yenye urefu wa Kilomita 2 kwa kiwango cha lami itatekelezwa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**245. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Ifumbo Chunya.



**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**246. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga soko la kisasa la mazao yatokanayo na uvuvi Wilayani Nkasi.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **247. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la kukatika kwa umeme katika Mji wa Mpwapwa.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA  
23 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**